



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANI
OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KIGOMA

(Barua zote zitumwekwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)



Tel. 028280 4865
Fax. 028280 2719/2370
Email: ded@kigomadc.go.tz
Tovuti: www.kigomadc.go.tz

Ofisi Ya Mkurugenzi Mtendaji,
S.L.P. 332,
KIGOMA.

Kumb. Na. KDC/HI/1/

Tarehe : 03 Desemba, 2024

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MKATABA

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Kigoma kwa kushirikiana na shirika la THPS imekuwa ikitekeleza Afua za kupambana na VVU/UKIMWI na Kifua kikuu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma . Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya Inakaribisha maombi ya kazi ya Muda (Miezi 12) kutoka kwa watanzania wenyewe Sifa, uwezo na Ujuzi wa taaluma za Afya. Mtumishi atapangiwa kufanya kazi katika Vituo vya Kutolea Huduma za Afya vilivyoopo katika Halmashauri ya Wilaya Kigoma. Nafasi inayotangazwa ni kama ifautavyo:

1. AFISA TAKWIMU (DATA OFFICER) – NAFASI 01

MAJUKUMU YA KAZI.

- I. Kuingiza takwimu kwa uharaka na usahihi zinazohusu matibabu kwenye CTC2 database.
- II. Kuandaa na kufanya mapitio ya takwimu za Afua mbalimbali za VVU/UKIMWI za kituo kwa wiki, mwezi na robo.
- III. Kufanya upembuzi na kuandaa orodha ya wagonjwa kwa ajili ya ufuatiliaji kama vile wateja waliopotea kwenye huduma, wateja ambao hawajahudhuria kwenye kliniki zao n.k
- IV. Kuwezesha upembuzi na tafsiri ya takwimu kwa ajili ya kupanga na kufanya maamuzi katika ngazi ya kituo
- V. Kutunza kumbukumbu za fomu na mafaili ya wateja kulingana na Miongozo.
- VI. Kufanya mlinganyo wa takwimu za Afua za VVU/UKIMWI zilizopo katika vyanzo mbalimbali vya taarifa.

SIFA ZA MWOMBADI.

- i. Awe mwenye Elimu na Cheti cha Kidato cha nne (IV) waliohitimu mafunzo ya AStashahada katika Fani ya Takwimu kutoka katika vyuo vinavyotambulika na Serikali na mwenye ujuzi wa kutumia kompyuta.

- ii. Astashahada, stashahada au zaidi kwa Sayansi ya Kompyuta, Habari za Afya, Takwimu au Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) au fani inayohusiana nayo.
- iii. Uzoefu usiopungua miaka miwili (2) wa kufanya kazi kama afisa wa uingizaji data katika mipangilio ya programu ya VVU/UKIMWI katika vituo vilivyopo Wilaya ya Kigoma.
- iv. Ujuzi wa uchambuzi na utatuzi wa changamoto.
- v. Uwezo wa kuwasiliana kwa ufasaha katika Kiingereza na Kiswahili.
- vi. Uwezo wa kufanya kazi kibinagsi na kama sehemu ya timu yenyewe usimamizi mdogo.
- vi. Uwezo wa kudumisha usiri katika nyanja zote.

MASHARTI YA JUMLA

I. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania.

II. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa,Maelezo binafsi(Detailed CV) yenye anuani na namba za simu pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.

III. Waombaji wote waambatanishe vyeti vya taaluma,nakala za vyeti vya kidato cha nne au sita kwa wale waliofika kiwango hicho.

IV. Testimonials"Provisional Results","Statements of Results", Hati za matokeoza kidato cha nne au sita (Form IV and Form VI Result Slips) Havitakubaliwa.

V. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE)

VI. Barua za maombi ya kazi ziandikwe kwa mkono Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya S.L.P 332 .**KIGOMA**. na kuwasilishwa kupitia barua pepe:afya@kigomadc.go.tz

VII. Watakaochaguliwa kufanya usahili watajulishwa kupitia njia ya simu na barua pepe.

VIII. Mwisho wa kupokea maombi ya kazi ni tarehe **10-12-2024** saa 09:30 Alasiri

LIMETOLEWA NA:


Chiriku Hamisi Chilumba
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KIGOMA.

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KIGOMA